JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S.L.P 42325,
Simu Nambari:
2850633
Nukushi: (022)
2850635
Barua Pepe:
rbctemeke@pccb.go.tz
Wavuti: www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

TEMEKE 22/04/2020

AFISA MIFUGO MBARONI KWA KOSA LA KUOMBA NA KUPOKEA RUSHWA.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Temeke katika kipindi cha mwezi Januari, 2020 hadi Machi, 2020 iliendelea na majukumu yake ya Kuzuia na Kupambana na rushwa kulingana na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007 na imefanikiwa kutekeleza mpango kazi wake katika Idara zote ikiwa ni pamoja na Uchunguzi, Uzuiaji Rushwa na Elimu kwa Umma.

Katika kipindi hicho, TAKUKURU Mkoa wa Temeke – Jijini Dar Es Salaam imepokea taarifa 109 zinazohusu vitendo vya rushwa, katika kipindi hicho Halmashauri ya Manispaa ya Temeke pamoja na taasisi binafsi zinaoongoza kwa kulalamikiwa. Katika taarifa hizo majalada mapya ya uchunguzi yaliyofunguliwa na kufika hatua ya uchunguzi wa kina ni majalada 6 na majalada mengine yanaendelea na uchunguzi katika hatua mbalimbali.

Katika kipindi hicho Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Temeke imeokoa kiasi cha Shilingi 270,927,922, fedha hizo zimeokolewa kutoka katika chunguzi mbambali kama vile fedha za SACOSS, fedha za mfuko wa Jimbo, fedha za ujenzi wa zahanati na miradi mbalimbali pamoja na fedha kutoka kwa wazabuni ambao hawakukatwa kodi ya zuio.

Aidha, TAKUKURU Mkoa wa Temeke kwa kipindi cha Mwezi Januari hadi Machi 2020 imefanikiwa kufungua kesi mpya 4 ambapo kesi ya kwanza ilifunguliwa mahakama ya Wilaya ya Temeke tarehe 06/01/2020 kesi namba CC/13/2020 na inamuhusu Bw. Issa William Nyanda na alifunguliwa mashitaka kwa kosa la kujifanya Afisa wa Serikali kinyume na kifungu cha 100(b) na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kinyume na kifungu cha 302 cha sheria ya kanuni za adhabu sura no. 16 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Kesi ya pili ilifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya ya Temeke tarehe 14/01/2020 kesi namba CC/33/2020 na inamhusu mfanyabiashara wa Duka la Dawa muhimu ambaye anafanya biashara zake katika mtaa wa Rangitatu Kata ya Charambe Bw. Ibrahim Rashid Kahenga kwa kosa la kufanya vitendo vya uzembe vinavyoweza kusababisha maambukizi ya magonjwa kinyume na kifungu cha 179 cha sheria ya kanuni za Adabu sura ya 16 kama iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002 na kuendesha Duka la madawa bila kibali kinyume na kifungu cha 34(1) na (5) cha Sheria ya Maduka ya Dawa na. 1 ya mwaka 2011 (Pharmacy Act No.1 of 2011).

Kesi ya tatu ilifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya ya Temeke tarehe 12/02/2020 kesi namba CC/01/2020 inayomhusu Afisa Mifugo kituo cha Bandari Dar-es-salaam anaejulikana kwa jina la Bw. Jovinus Julius Lukonge kwa kosa la kuomba na Kupokea Rushwa kinyume na kifungu cha 15(1) (a) cha sheria ya Kuzuia Na Kupambana na Rushwa na.11 ya mwaka 2007.

Aidha uchunguzi umethibitisha kuwa siku ya tarehe 06/09/2019 Bw. Jovinus Julius Lukonge aliomba hongo ya kiasi cha Tsh. 400,000/= ili aweze kumpunguzia mlalamikaji ushuru/ kodi aliyopaswa kulipa baada ya kuingiza mzigo wa maziwa kutoka Zanzibar na kumgongea muhuri utakaothibitisha kwamba bidhaa hizo zimekaguliwa na zipo salama kwa matumizi ya binadamu. Mtuhumiwa ametenda kosa kinyume na kifungu cha 15(1) (a) cha sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na.11 ya mwaka 2007.

Kesi ya nne ilifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kigamboni tarehe 17/01/2020 kesi namba CC/03/2020 na inamhusu Josephine Jilles Nchinga ambaye ni Karani Mahakama ya Wilaya ya Kigamboni na aliyekamatwa kwa kosa la kuomba na kupokea Rushwa kiasi cha

shilingi 300,000/= Kinyume na Kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na. 11 ya mwaka 2007. Hadi sasa kesi zinazoendelea Mahakamani ni nane (8).

TAKUKURU iliendelea na jukumu la kuelimisha umma kupitia njia mbalimbali, lengo likiwa ni kuwahamasisha wananchi kushiriki kwa vitendo katika mapambano dhidi ya rushwa. Uelimishaji ulifanywa kwa kuendesha semina 11 kwa makundi mbalimbali na mikutano ya hadhara 5 kwa wananchi. Pia, tumetoa kipindi 1 cha elimu ya mapambano dhidi ya rushwa katika Redio na kipindi kimoja (1) katika Televisheni, ambapo mkazo mkubwa uliwekwa kwenye elimu dhidi ya rushwa kwenye uchaguzi na kudhibiti rushwa ya ngono. Pia katika kusheherekea siku ya wananwake duniani tumeshiriki katika shughuli moja (1) ya kijamii.
Aidha, katika kuandaa Taifa la vijana wanaoichukia rushwa, vilabu kumi (10) vya wapinga rushwa vilifunguliwa katika shule za msingi na sekondari na vilabu vitano (5) vya zamani zilitembelewa kwa lengo la kuviimarisha.

Katika kipindi hicho tumefanya chambuzi za mfumo mbili (2) kwa lengo la kubainisha mianya ya rushwa na kisha kudhibiti mianya hiyo kwa kutoa ushauri na mapendezo kwa mamlaka zinazohusika. Chambuzi hizo zilihusisha uchambuzi wa mfumo kuhusu uendeshwaji wa miradi ya maji katika Halmashauri ya wilaya ya Temeke na uchambuzi wa mfumo wa vyama vya ushirika (AMCOS) katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni.

Pia Dawati la Kuzuia Rushwa limefanya ufuatiliaji wa maazimio (Compliance) nne (4) kwa makubaliano yaliyofanyika kwenye warsha ya makusanyo ya Mapato katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni, warsha ya manunuzi ya umma katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni warsha ya Makusanyo ya Mapato katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke na warsha kuhusu elimu msingi bure (Capitation grants) kwa shule za msingi katika Halmashauri ya wilaya ya Temeke.

Miradi ya maendeleo 7 yenye thamani ya Tsh. 15,475,628,712.5 imefanyiwa ufuatiliaji na kutolewa ushauri kwa lengo la kufanya marekebisho kwa lengo la kupata thamani ya fedha. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo;

Mradi wa ujenzi wa madarasa 20 na vyoo 10 vya shule ya Sekondari Mbagala wenye thamani ya Shilingi 400,000,000/=. Mradi wa ujenzi wa madarasa 8 ya shule ya Sekondari Minazini wenye thamani ya shilingi 160,000,000/. Mradi wa madarasa 8 kwa shule ya Sekondari Kibasila wenye thamani ya Tsh 160,000,000/= Mradi wa matengenezo ya barabara (periodic maintenance and spot improvement) wa kongowe – mjimwema – kivukoni Road wenye thamani ya shilingi 1,587,729,062.50/=. Mradi wa ujenzi wa soko la kisasa Kibada wenye thamani ya Shilingi 13,030,384,450.00/=. Mradi wa ujenzi wa madarasa mapya ya shule ya Sekondari Kigamboni (Kivukoni) wenye thamani ya shilingi 100,000,000/=. Mradi wa upanuzi wa jengo la maabara hospitali ya vijibweni Manispaa ya Kigamboni wenye thamani ya shilingi 37,515,200/=.

Takukuru (M) Temeke imeweka mikakati ya kipindi cha Aprili-juni 2020 ya kudhibiti vitendo vya Rushwa katika Mkoa wetu na kuangalia njia bora ya kuweza kutokomeza vitendo vya Rushwa katika miradi mbalimbali iliyopo katika Manispaa ya Temeke ikiwemo miradi ya Elimu, Maji, Ujenzi wa miundo mbinu, Ukusanyaji wa mapato na manunuzi ya umma, Maliasili na Utalii, Madini, Viwanda, Biashara, (kuimarisha mazingira ya biashara), uwekezaji pamoja na miradi ya Kilimo, mifugo na ushirika, Aidha tunayo mikakati ya kuelekea kipindi cha uchaguzi mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba kwa kuelimisha wananchi kupitia njia mbalimbali ikiwemo kufanya mikutano ya hadhara, semina kwa wagombea pamoja na mawakala ili kudhibiti vitendo vya rushwa katika kipindi cha uchaguzi.

TAKUKURU (M) Temeke inaendelea kutoa wito kwa wananchi wote kuchukua tahadhari na kutoa taarifa pale wanapopigiwa simu na kuombwa fedha na watu ambao wanajifanya maafisa wa TAKUKURU kwani vitendo hivyo ni kinyme na sheria, vile vile tunatoa wito kwa wananchi kutoa ushirikiano katika kufichua vitendo vya rushwa kwa kupiga simu ya dharura namba 113 au kufika ofisi za TAKUKURU, kwani kwa kufanya hivyo tutaitokomeza kabisa rushwa na kuinua zaidi uchumi wa nchi yetu.

KUPAMBANA NA RUSHWA NI JUKUMU LANGU.

DONASIAN KESSY,
MKUU WA TAKUKURU (M) TEMEKE